

**LEARNING BY EAR 2011****“The Promised Land- A Story of African Migration to Europe”****EPISODE FIVE: “Is My Skin My Sin?”****AUTHOR: Chrispin Mwakideu****EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann****KISUAHELI: Eric Ponda****List of characters by scene:****SCENE ONE: LINDA AT THE SECURITY GATE**

- Linda (f, 20)
- Security officer (m, 40)
- Airport announcer (m/f, 35)

**SCENE TWO: FARAHANI AND SULE TALK TO SULE'S FATHER HAMAD**

- Farahani (m, 19)
- Sule (m, 19)
- Hamad (m, 60)

**SCENE THREE: LINDA AND FLORENCE HAVING A DRINK AT THE EUROPEAN AIRPORT**

- Linda (f, 20)
- Florence (f, 35)

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”- Episode 5

- **Mr. Maraga**

## **SCENE FOUR: ENCOUNTER BETWEEN FRONTEX AND ILLEGAL MIGRANTS AT SEA**

- **Frontex Guard (m, 40)**
- **Farahani (m, 25)**
- **Small crowd of migrants**

### **INTRO:**

Hujambo na karibu kwa sehemu ya tano kwenye mfululizo wa mchezo huu wa Redio Noa Bongo Jenga kwa Jina “**Ardhi ya ahadi - hadithi kuhusu Waafrika wanaohamia Ulaya.**”. Katika kipindi kilichotanguli, Farahani aibuka na wazo jingine la kuingia kisiri Ulaya kwa kutumia mashua ndogo ya Babake Sule.

Linda, naye yuko katika mkondo wa mwisho kuelekea Ulaya kujiunga na chuo kikuu. Tayari tofauti za kiutamaduni zinabainika kuwa changamoto kubwa ya kwanza kwa Linda anapowasili uwanja wa Ndege barani Ulaya. Bado anajaribu kutafuta lango la kuondoka uwanja huo wa ndege. Je atafaulu kuondoka kwa wakati uafao? Endelea kuwa nasi katika kipindi hiki , “**Ngozi yangu dhambi zangu.**” Kwanza tunakutana na Linda akikaguliwa kwenye mtambo wa ukaguzi wa usalama katika uwanja huo wa ndege.

## **SCENE ONE: LINDA AT THE SECURITY GATE**

1. **SFX: BEEPING SOUND AS WHEN METAL DETECTOR DETECTS METAL**

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”- Episode 5

**2. SECURITY:** Rudi rudi nyuma, sasa jaribu tena kupita,..ukiwa umetoa kila kitu kilichoko kwenye mfuko wako,..sarafu, mkufu, vipuli na chochote cha chuma.

### **3. SFX: JINGLING OF COINS PLACED IN TRAY**

**4. ANNOUNCER:** **(via speakers)** Kwa mara ya mwisho,Bi Linda Maraga tafadhali! Bi Linda Maraga! Tayari shughuli ya kuabiri ndege imekamilika. Fika haraka kwenye lango nambari tano la sivyo mizigo yako itashukishwa kwenye ndege.

**5. LINDA:** **(in tears)** Tafadhali hilo ni jina langu ..,tafadhali...!

**6. SECURITY:** **(in a rush)** Sasa unasubiri nini? Pita uende! nenda!

### **7. SFX: FUMBLING WITH PERSONAL BELONGINGS**

**8. LINDA:** **(panicking and in a rush)** Mungu wangu nisaidie! Nisikose ndege – siwezi..

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”- Episode 5

**9. NARRATOR:**Haraka haraka Linda anakusanya mizigo yake na kuelekea lango la kuondoka uwanja wa ndege.Maombi yake yamepokewa kwani anafika na kuabiri ndege kwa wakati ufaao! Na anapochukua nafasi yake kuketi, anakutana tena na Florence. Hii ni afueni kubwa kwake!.Na bila ya kusita anamueleza changamoto alizokumbana nazo katika uwanja huo wa ndege. Lakini kabla kusikia kutoka kwa Folorence, hebu twende moja kwa moja kuungana na Farahani na rafiki yake Sule wakiwa bandarini wakijaribu kumshawishi babake Sule, Mzee Hamad kuhusu mpango wao.

## **SCENE TWO: FARAHANI AND SULE TALK TO SULE'S FATHER HAMAD**

**10. SFX:** sea breaking on the shore, harbour noise, e.g. people unloading their boats, busy talking, seagulls

**11. FARAHANI:** (calming) Usiwe na hofu Mzee Hamad. Punde tutakapowasili Ulaya na kuanza kufanya kazi tutakununulia mashua nzuri zaidi. Zile mashua kubwa zenye injini,..! na hata unaweza kulala ndani mvua inaponyesha. Si unazijua mashua hizo?.

**(Silence)**

**12. HAMAD:** (clears throat) Sule, wewe na rafiki yako munawazimu!, kuja kwangu kuniomba mashua inayotegemewa na familia yangu?. Ya kazi gani? Eti kwa sababu mnataka kutimiza ndoto yenu ya kuhamia nchi ya wazungu.? Nini kinachowavutia

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”- Episode 5  
nyinyi vijana katika nchi hizi za Ulaya.?

**13. SULE:** **(whispering)** Farahani, nimekuonya kwamba Babangu hatakubaliana nasi.

**14. HAMAD:** **(shouting)** Nyamaza wakati mimi nazungumza!. Umekosa adabu!. Haya ndiyo mambo munaenda kujifunza huko Ulaya?Sasa nisikilize kwa makini!. Ni miaka 12 tangu nianze kazi hii ya baharini. Bahari si uwanja wa kuchezea! Na Mashua yangu si kikaragosi! Niondokeeni haraka!

**15. FARAHANI:** Mzee Hamad, labda hujanielewa sababu ya... -

**16. SFX: BOAT HIT HARD BY A WALKING STICK**

**17. HAMAD:** **(furious)** Niondokee harahaka! Ondoka! Kabla sijakucharaza kiboko! Badala ya kutafuta kazi mkafanya, mkauoa na kuanza familia, nyinyi mnaota kuhamia Ulaya na kujenga kasri baharini.

**18. FARAHANI:** **(frustrated)** Kwenye hewa...! Umekosea Mzee Hamadi! Ni kujenga Kasri hewani sio baharini.

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”- Episode 5

**19. NARRATOR:** Farahani anaodnoka na kumuacha Mzee Hamadi Bandarini. Japo hajakasirika lakini ameghadhabika sana. Je ndoto yake ya kwenda Ulaya ndiyo imegonga mwamba? Lakini sasa tumugeukie Linda na Florence. Baada ya safari yao fupi wanawasili wanakokwenda. Bado Linda anapitia utaratibu ule wa ukaguzi katika idara ya uhamiaji kabla ya kuondoka uwanja wa ndege. Lakini hatimaye amewasili salama na Florence anamualika kikombe cha Chai.

### **SCENE THREE: LINDA AND FLORENCE HAVING A DRINK AT THE EUROPEAN AIRPORT**

**20. SFX: CAFE ATMO / AIRPORT**

**21. LINDA:** **(exhausted)** Florence, siamini niliyopitia sasa hivi. Safari hii imekuwa ngumu sama. Kamwe sikudhania mambo yatakuwa kama nilivyoshuhudia. Watu ni wajeuri, na yaonekana kana kwamba hawaniamini hata ninapozungumza nao.

**22. FLORENCE:** Karibu Ulaya! Nilikuwa na rafiki yangu kutoka Africa hapa Ulaya ambaye alikuwa akiniambia, “Ngozi yangu ndiyo Dhambi zangu”.

**23. LINDA** Kumaanisha?

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”- Episode 5

**24. FLORENCE:** Kumaanisha, ngozi yetu ndiyo chanzo cha kudharauliwa. Japo si wote walio na ubaguzi wa rangi. Kama wangukuwa hivyo singeolewa na Mzungu mimi.! **(laughs)** Pole sana kwa usumbufu uliopitia katika siku yako ya kwanza. Siku hizi watu ni wamekuwa waoga kutokana na tisho la mashambulizi ya kigaidi. Lakini mbali na hayo wenyewe si wakarimu kama jamaa zetu nyumbani. Lazima kwanza uizoe hali hii.

**25. LINDA:** **(embarrassed)** Flo! Nakushuruku sana kwa ushauri wako. Eee...samahani, sitaki yawe mazoea, lakini naweza kuomba nitumie simu yako? Nataka kuwatuma ujumbe kwa wazazi wangu kuwajulisha kwamba nimefika salama, ili wasiwe na wasi wasi.

**26. FLORENCE:** Hakuna neno. Tumia tu!. Wapigie! Nahakika watafurahi sana kusikia sauti yako.

**27. LINDA:** Asante sana, Flo! Wewe ni rafiki mzuri !

## **28. SFX: DIALLING OF NUMBERS ON A MOBILE PHONE**

**29. MR. MARAGA:** **(answers call)** Hello...Ni Nani?

**30. LINDA:** **(thrilled)** Baba, ni mimi Linda.

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”- Episode 5

**31. MR. MARAGA:** Linda! Oh, Mungu ni mkubwa!Unaendeleaje.? umefika salama? Hii ni nambari ya nani?

**32. LINDA:** Niko salama Baba. Natumia simu ya rafiki yangu. Safari ilikuwa salama tu japo wasi wasi na matatizo kidogo ya hapa na pale. Kidogo ningeachwa na ndege. Watu huku si wakarimu kama nyumbani . Lakini Ulaya ni kuzuri sana!.

**33. SFX: BAD CONNECTION ON THE LINE**

**34. MR. MARAGA:** Hello! Linda? Sikusikii vizuri. Unapigia ukiwa wapi?

**35. LINDA:** Samahani Baba, muda umekwisha, Musalimia sana Mama, na mwambie nimefika salama. Nawatamani sana...!

**36. MR. MARAGA:** Hello? Helloooo... Linda, uko huko ?

**37. SFX: BEEP OF MOBILE PHONE CALL BEING ENDED**

**38. LINDA:** Asante sana, Flo!. Sasa wazazi wangu hawana wasi wasi tena baada ya kuwafahamisha nimefika salama.

**39. FLORENCE:** Linda, Ningependa kukupa ushauri... Usijaribu kuwaeleza watu nyumbani kuhusu ugumu wa maisha huku,wala matatizo unayopitia.Hata ikiwa ni shida ya aina gani ..! Usijaribu kuwaelezea ukweli.

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”- Episode 5

**40. LINDA:** **(surprised)** Nini?! Kwani nini, Florence? Hawa ni wazazi wangu, wanahaki ya kujua kinachoendelea au matatizo yanayonipata!

**41. FLORENCE:** **(sympathetic)** Mmm... Silazima nikupe sababu Linda. Zingatia niliyokwambia. Jaribu kushughulikia matatizo yako mwenyewe !

**42. SFX: MOBILE PHONE RINGING**

**43. FLORENCE:** Oh – Sasa nataka kwenda. Tayari dereva wangu amefika. Shika hizi yuro 20 utalipa chai na uweke bakshishi. Nimekupa nambari yangu ya simu nipigie wakati wowote ukiwa na shida, nimefurahi sana kukutana na wewe Linda. Kwaheri.

**44. SFX: LUGGAGE BEING WHEELED AWAY**

**45. NARRATOR:** Linda anamtazama Florence akisukuma troli yake ya mizigo kuelekea sehemu ya kuegesha magari. Na kwa mara ya kwanza kabisa Linda anajihisi pweke na muoga sana. Anatazama huko na kule angalau kama naweza kumuona mtu anayemfahamu lakini wapi!... sura zote ni ngeni kwake! Analipia chai na kufululiza hadi kituo cha Gari moshi na kuabiri garimoshi kuelekea chuoni. Sasa tuachane na Linda kidogo anapoanza maisha yake mapya, na tugeukie Farahani huko Africa Kaskazini. Baada ya Mzee Hamad, kukatalia na mashua yake, Farahani anaamua kuungana na wahamiaji wengine wanaojaribu kuingia Ulaya kisiri wakitumia mashua ndogo wanamosongamana. Safari hii amekuwa msiri sana, hajamueleza Mtu yoyote kuhusu mipango yake.- Hata rafiki yake Sule. Baada ya siku kadhaa baharini, Farahani na wenzake

Learning by Ear 2011 “The promised land – A story of African migration to Europe”- Episode 5  
wanakaribia ufuo wa Bara Ulaya...

**SCENE FOUR: ENCOUNTER BETWEEN FRONTEX AND ILLEGAL  
MIGRANTS AT SEA**

**46. SFX: ROUGH SEA WAVES HITTING ON BOAT**

**47. FRONTEX GUARD: (via megaphone)** Sisi ni walinzi wa fuo za Habari hii ya Ulaya. Tafadhali mnahitajika kuwa watulivu. Na msijirushe baharini. Kuanzia sasa mko chini ya ulinzi wa maafisa wetu watakao msindikiza.

**48. FARAHANI: (shouts)** Kutupeleka wapi? Tunataka kwenda Ulaya. Tunafahamu kwamba tunakaribia na hata tunaweza kuona fuo za Ulaya.

**49. FRONTEX GUARD: (via megaphone)** Tumekamata mashua yenu katika maji ya bahari ya Afrika, na tutawarejesha salama baada ya kubainika mnakotoka.

**50. FARAHANI:** Hapana hatutaki kurudi huko!. Hatuna stakabadhi!. Sisi si raia wa taifa lolote!

**51. FRONTEX GUARD:** Sawa tutajua hayo baadaye. Tunafahamu kwamba mnajaribu kuingia Ulaya kinyime na sheria, na jukumu letu sisi kama walinzi wa mipakani ni kuhakikisha mipaka yetu iko salama. Tafadhali tunaombe mshirikiane nasi kwa usalama wenu.

**52. FARAHANI:** (adamant) Siwezi kurudi. Sitarudi! Hamuwezi...!

### 53. SFX: FARAHANI DIVES INTO THE SEA

**53.a FRONTEX GUARD:** **(shocked)** Ahh...! amejirusha baharini! Haraka umuokoe, kuna mawimbi makali sana asije akafa maji!

### 54. SFX: MIGRANTS MAKING SHOCKED AND SCARED EXCLAMATIONS

**55. FARAHANI:** **(drowning)** Nisaidieni,!.. Nisaidieni....!

### 56. SFX: TWO MORE PEOPLE DIVE INTO SEA

**57. FRONTEX GUARD:** Umempata? Yuko salama? **(deep breath)** Okay. Sasa sikilizeni kwa makini. Hatuwezi kuwadhuru, tafadhali kila mmoja atulie na mambo yatakuwa shwari.

### OUTRO:

Farahani anaokolewa baharini na walinzi wa maafisa wa usalama baharini na kurejeshwa Afrika alikotoka kinyume na matakwa yake. Lakini bado hajakata tamaa... Je anamipango gani ya baadaye? Na hadi hapo ndipo tunafika mwisho wa sehemu hii ya tano ya mfululizo wa mchezo huu “**Ardhi ya Ahadi**” kuhusu **Wafrika wanaohamia Ulaya**. Ungana nasi kwenye kipindi kinachofuata usikia jinsi Linda anavyokabiliana na changamoto za masomo barani Ulaya. Pia naweza kukisikiliza tena kupitia mtandao wetu wa [dw.de/destinationeurope](http://dw.de/destinationeurope). Kwaheri kwa sasa!